# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia uzima na afya na tukaweza kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa hotuba hii ni kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 109 (15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambayo inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza katika Mkutano wa mwezi wa Febuari au wakati mwengine ambapo Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza itaamua.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti hutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza. Aidha, Kamati huzingatia Katiba, Sheria na miongozo mbali mbali ya nchi katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara mbali mbali, Taasisi, Mamlaka, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya kupokea taarifa za utendaji kazi na kupokea maoni mbali mbali. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa Serikali na taasisi hizo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi pamoja na utekelezaji bora wa bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imeundwa na Wajumbe nane (8) na Makatibu Kamati wanne (4) kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mwanaasha Kh. Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Dkt.Soud Nahoda Hassan | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Suleiman Masoud Makame | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Abass Vuai Moh'd | Katibu |
| 10. | Ndg. Asha Said Muhammed | Katibu |
| 11. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 12. | Ndg. Shaib Fadhi Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Kamati ya Bajeti imegawika katika Sehemu Kuu nane (8). **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi, **Sehemu ya Pili** ni Tathmini ya Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi Zanzibar, **Sehemu ya Tatu** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na Nusu Mwaka wa fedha 2023/2024 (Julai – Disemba 2023/2024), **Sehemu ya Nne** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa kipindi cha Julai- Disemba kwa mwaka 2023/2024, **Sehemu ya Tano** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Taasisi na Mashirika ya Umma, **Sehemu ya Sita** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Programu mbali mbali, **Sehemu ya Saba** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, na **Sehemu ya Nane** ni Hitimisho.

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika;** Mfumko wa Bei Zanzibar umekuwa wa wastani katika miaka ya hivi karibuni. Katika mwaka 2023 mfumko wa bei Zanzibar umefikia asilimia 6.9. Mwaka 2022, mfumko wa bei ulikuwa asilimia 5.1, ikilinganishwa na mfumko wa bei wa asilimia

1.7 mwaka 2021. Ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kwamba mfumko wa bei utaendelea kudhibitiwa ili uendelee kuwa wa wastani na wa tarakimu moja katika miaka ya ijayo.

**Mheshimiwa Spika;** Miongoni mwa sababu zilizosababisha Mfumko wa Bei ni kutegemea bidhaa nyingi kutoka nje. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na kuweka mikakati mahsusi ya kuimarisha uzalishaji wa ndani ili kupunguza utegemezi wa uagizaji hususan kwa zile bidhaa ambazo tunaweza kuzalisha katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;** Vile vile, Kamati inaishauri Serikali, kuendelea na juhudi madhubuti za kuzalisha ajira kama vile kuimarisha mfumo wa mafunzo ya amali ili kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi ambao unahitajika katika sekta za uzalishaji, kukuza maendeleo ya viwanda vya ndani ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma, na kuimarisha mazingira ya biashara ili kufanya iwe rahisi kwa kampuni kuanzisha na kufanya biashara Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania, Thamani ya Shilingi ya Tanzania imepungua dhidi ya sarafu nyingine za kigeni katika miezi ya hivi karibuni. Hii inasababisha ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kutokana na upungufu wa Dola ya Marekani. Kamati inaipongeza Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha upatikanaji wa fedha hizo za kigeni ili kuwasaidia wafanyabiashara kuweza kuagiza bidhaa muhimu nje ya nchi hususan ambazo hazizalishwi katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Utalii imeendelea kukua siku hadi siku hali inayopelekea idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar kuongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni. Mwaka 2023, idadi ya watalii ilikuwa 638,498, ikilinganishwa na 544,233 mwaka 2022. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kwa kiasi kikubwa kunachangiwa na juhudi za Serikali katika kuitangaza Zanzibar sambamba na kujenga miundombinu bora na kuimarisha huduma kwa watalii. Kamati inaishauri Serikali, kuongeza kasi zaidi na kuweka usimamizi bora uimarishaji wa miundombinu ya msingi, kama vile barabara, viwanja vya ndege, na bandari. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya utalii na hatimae kuzidi kutoa mchango katika Pato la Taifa.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 NA NUSU MWAKA WA FEDHA 2023/2024 (JULAI – DISEMBA 2023/2024)

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 2,572.7 bilioni na mapato halisi yalikuwa TZS 1,590.3 bilioni sawa na asilimia 61.8 ya makadirio ya mapato. Serikali imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato halisi kwa asilimia 10.8 ikilinganishwa TZS 1,434.9 bilioni zilizokusanywa mwaka wa fedha uliopita wa 2021/2022. Ukuaji huu wa mapato uliwezeshwa na ukuaji wa uchumi, pamoja na hatua mbali mbali za Serikali za kuongeza mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa matumizi, Serikali ilipanga kutumia jumla ya TZS 2,572.7 bilioni, ikiwa ni pamoja na TZS 1,220.5 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na TZS 1,352.2 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hata hivyo, matumizi halisi yalikuwa TZS 1,453.7 bilioni. Kati ya kiasi hicho, TZS 993.0 bilioni zilitumika kwa matumizi ya kawaida, na TZS 460.7 bilioni zilitumika kwa matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Ili kuwa na utekelezaji mzuri wa bajeti, Serikali inapaswa kuimarisha sekta binafsi na kuipa nguvu ili kuongeza uzalishaji wa ndani ambao utaongeza mapato ya Serikali. Hatua hii itasaidia kupunguza nakisi ya bajeti kwa kuimarisha mapato ya ndani. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea na juhudi za kuimarisha nidhamu ya matumizi kwa taasisi za umma ili kudhibiti uvujaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 2,572.7 bilioni na mapato halisi yalikuwa TZS 1,590.3 bilioni sawa na asilimia 61.8 ya makadirio ya mapato. Serikali imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato halisi kwa asilimia 10.8 ikilinganishwa TZS 1,434.9 bilioni zilizokusanywa mwaka wa fedha uliopita wa 2021/2022. Ukuaji huu wa mapato uliwezeshwa na ukuaji wa uchumi, pamoja na hatua mbali mbali za Serikali za kuongeza mapato ya ndani. Aidha, Serikali ilipanga kutumia jumla ya TZS 2,572.7 bilioni, ikiwa ni pamoja na TZS 1,220.5 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na TZS 1,352.2 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hata hivyo, matumizi halisi yalikuwa TZS 1,453.7 bilioni. Kati ya kiasi hicho, TZS 993.0 bilioni zilitumika kwa

matumizi ya kawaida, na TZS 460.7 bilioni zilitumika kwa matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Bajeti inafarijika kuona Serikali inaongeza fedha za kazi za maendeleo mwaka hadi mwaka ili kuimarisha miundombinu ya msingi, elimu na afya. Katika kipindi hiki, Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara kuu na za ndani, ujenzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa miundombinu ya maji na nishati. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizi.

**Mheshimiwa Spika;** Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa nusu mwaka wa fedha 2023/2024, kumekuwepo na baadhi ya changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa mfumko wa bei, ambao uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2022 hadi kufikia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2023. Ukuaji huu wa mfumuko wa bei ulisababishwa na kupungua kwa thamani ya fedha za umma, na hivyo kusababisha ongezeko la gharama za miradi ya maendeleo. Changamoto nyengine ni kupungua kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ambayo inatumika sana kununua bidhaa nje ya nchi. Changamoto hii imesababishwa na upungufu wa upatikanaji wa Dola ya Marekani katika masoko ya kubadilisha fedha.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kutatua changamoto hizo nilizozitaja, Kamati yangu inaishauri Serikali iendelee kuongeza mapato ya Serikali kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Kwa kiasi kikubwa, ukusanyaji wa mapato ya kodi umeimarika jambo ambalo Kamati inaipongeza sana Serikali. Lakini ipo haja sasa, Serikali kuweka mikakati katika kuimarisha mapato yasiyokuwa ya kodi.

**Mheshimiwa Spika;** Kuhusu Deni la Taifa, Hadi kufikia Disemba 2023, Deni la Taifa lilikuwa TZS 820.0 bilioni na kwa upande wa Deni la Nje linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi kufikia Disemba, 2023 lilikuwa TZS 2,562.8 bilioni. Deni la Taifa la Zanzibar limekuwa likiongezeka kutokana na sababu mbali mbali, ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika miradi ya maendeleo. Serikali imewekeza sana katika miradi ya maendeleo katika miaka ya hivi karibuni, na hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za Serikali. Sababu nyengine ni kiwango cha mapato ya ndani

bado hakitoshelezi kugharamia miradi ya maendeleo. Hii inasababisha Serikali kutegemea misaada na mikopo ya nje ili kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba mikopo hii inatumika kwa ufanisi na weledi ili iweze kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo itasaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imejumuisha mafungu makuu sita (6) ambayo ni OR- Fedha na Mipango F01, Mfuko Mkuu wa Serikali F02, Tume ya Mipango F03, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali F04, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali F05 na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali F06. Mafungu hayo yanaundwa na Idara ishirini na tatu (23), Taasisi saba (7) na Ofisi tano (5) za Pemba.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ilikadiriwa kukusanya TZS 2,768 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 11 ya makadirio ya kukusanya TZS 2,498 bilioni ya mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imekusanya TZS 1,611 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,688 bilioni. Aidha, matumizi yalikuwa ni TZS 169.689 bilioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya kutumia TZS 193.474 bilioni.

### Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kipindi cha Julai - Septemba 2023/2024

### Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, ZRA imeweza kukusanya TZS 351.768 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 104.89 ya makadirio ya TZS 335.382 bilioni. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa kuendelea vizuri kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, ongezeko la wageni walioingia nchini, usimamizi imara wa ukusanyaji wa mapato hayo, kuimarika kwa huduma zinazotolewa na ZRA na kuongezeka kwa ufanisi wa watendaji wa ZRA. Aidha, matumizi ya ZRA katika kipindi hichi Julai - Disemba 2023/2024 ni matumizi ni TZS 9.296 bilioni sawa na asilimia 71.21 ya makadirio ya kutumia jumla ya TZS 14.28 bilioni.

**Mheshimiwa Spika;** ZRA imekuwa ikifanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato, Kamati inaipongeza sana Serikali na ZRA kwa mafanikio wanayoendelea kupata. Aidha, kwa lengo la kuendelea kuongeza mapato, Kamati inashauri ZRA kuongeza mashirikiano na walipa kodi kwa kuandaa mabonanza ya michezo na walipa kodi, kuandaa tafrija za utoaji tuzo kwa walipa kodi bora, kuandaa makongomano, semina na mikutano kwa ajili ya kuwapa elimu wafanyabiashara ya namna ya kutelekeza wajibu wa kulipa kodi lakini pia namna ya kukuza biashara zao. Kuimarika kwa biashara za wafanyabiashara hawa zitaongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Vile vile Kamati inaishauri ZRA kuendelea kuimarisha ushirikiano na walipa kodi sambamba na kuongeza ufahamu wa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri ZRA iongeze mashirikiano na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili kupunguza utoaji wa pesa taslimu Zanzibar. Hatua hii itasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa ukwepaji wa ulipaji kodi.

## Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar

**Mheshimiwa Spika;** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, TRA - Zanzibar imekusanya TZS 253.394 bilioni dhidi ya makadirio ya kukusanya TZS 253.933 bilioni hii ni sawa na ufanisi wa asilimia 99.8 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imeelezwa kwamba, katika mwezi Desemba 2023, TRA - Zanzibar ilifanikiwa kuweka rekodi kwa kukusanya kiasi cha TZS 62.941 bilioni. Hii ni rekodi mpya tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo. Kamati ya Bajeti inaipongeza sana TRA - Zanzibar kwa mafanikio haya, na ni imani ya Kamati kwamba itaongeza juhudi zitakazowezesha kufanya vizuri zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika;** Licha ya mafanikio hayo ya TRA – Zanzibar, Kamati imebaini yapo maeneo ambayo yakiimarishwa zaidi mapato yataendelea kuimarika kila siku. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutafuta ufumbuzi wa haraka changamoto ya uchelewaji wa kutatua migogoro ya kodi katika ngazi ya Mahakama za kodi kutokana na kesi zinazotokea baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Walipa Kodi mbali mbali. Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango isimamie kwa karibu suala la utatuzi wa migogoro ya kodi katika ngazi za Mahkama za kikodi kwa kuhakikisha watendaji wanaohitajika kuwepo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi wanapatikana kwa wakati ili kesi zinaposikilizwa ziweze kufikia katika maamuzi ya mwisho na kuifanya TRA na Walipa kodi kufikia kwenye maamuzi sahihi ya malalamiko yao iwapo yatajitokeza kutoka katika pande zote mbili.

## Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

**Mheshimiwa Spika;** Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024 ilikusanya jumla ya TZS 85.980 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 26 ya kipindi kama hicho kwa mwaka 2022 ambapo mapato ya PBZ yalikuwa TZS 68.164 bilioni. PBZ imefanikiwa kuvuka malengo ya kukusanya TZS. 74.491 bilioni sawa na ongezeko asilimia 15 ya mapato halisi. Kamati inaipongeza PBZ kwa kuweza kuvuka malengo ya ukusanyaji na pia Kamati inaitaka PBZ kuendelea na kasi hiyo pamoja na kuwapa motisha wafanyakazi wake. Aidha, kwa upande wa matumizi ya PBZ kwa

kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024 yalikuwa TZS 46.231 bilioni. PBZ imefanikiwa kudhibiti matumizi ukilinganisha na makadirio ya kutumia TZS 49.535 bilioni kwa asilimia 7.

**Mheshimiwa Spika;** mbali na mafanikio hayo, PBZ inakabiliwa na changamoto mbali mbali kama vile kuwepo mapungufu ya matumizi ya teknolojia kama vile kutokufanya kazi mashine za ATM mara kwa mara Pamoja na kutokufanya kazi mfumo wa PBZ Mobile. Katika hili Kamati inaishauri PBZ kuendelea kuimarisha vitengo vyake vya TEHAMA, kuimarisha bidhaa na huduma zake kuwa za kisasa ili kukidhi mahitaji ya wateja wake.

**Mheshimiwa Spika;** Changamoto nyengine inayoikabili PBZ ni kuongezeka kwa ushindani na benki nyingine za kibiashara na kuwepo kwa huduma kwa wateja zisizoridhisha. Wateja wengi hulalamika kwa kuchukua muda mrefu sana kupatiwa huduma katika matawi na vituo vya kutolea huduma vya PBZ. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za kuimarisha PBZ ili iweze kujiendesha kibiashara na hatimae kushindana na benki nyengine kama vile CRDB, NMB, NBC.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati pia inaishauri PBZ kutengeneza mpango maalum wa kutoa mafunzo kwa watendaji wote wa PBZ hususan watendaji wa huduma kwa wateja kuhusu namna ya kushughulikia malalamiko ya wateja kwa njia ya kirafiki na ya kusaidia, pamoja na kuweka utaratibu wa kufuatilia malalamiko ya wateja ili kuhakikisha kuwa yanashughulikiwa kwa wakati na kwa ufanisi. Hii inaweza kusaidia PBZ kujenga uaminifu kwa wateja wake na kupunguza idadi ya malalamiko ya wateja.

### Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA)

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 365 milioni na kuweza kukusanya TZS 255.06 milioni sawa na wastani wa asilimia 70 ya makadirio. Aidha, Mamlaka imejipangia kutumia TZS 1.28 bilioni na kuingiziwa TZS 1.02 bilioni sawa na asilimia 79.7. Kati ya fedha hizo TZS 809.37 milioni kwa ajili ya mishahara na TZS 219.9 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kukabiliana na changamoto ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika utumiaji wa mfumo wa manunuzi kwa baadhi ya taasisi. Kamati inaishauri Mamlaka ya Manunuzi iendelee kutoa mafunzo kwa taasisi za Serikali ili kuondosha changamoto katika matumizi ya mfumo wa manunuzi na hatimae kuleta ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za taasisi. Suala la utoaji wa mafunzo liwe endelevu kila inapohitajika ili lengo la kuanzishwa mfumo huu lipatikane.

## Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) limefanikiwa kukusanya TZS 19.5 bilioni ya mauzo ya bima ambayo ni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya kukusanya TZS 22.6 bilioni. Aidha, Shirika la Bima lilitumia TZS 3.9 bilioni kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa Ofisi, TZS 2.38 bilioni zimetumika kulipa madai mbali mbali ya wateja wake waliopata ajali na kutimiza matakwa ya sheria za bima, na TZS 1.7 bilioni zimetumika pia kulipa ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kuimarisha Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Kamati inaishauri Serikali ianze utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watendaji wa umma kuhusu umuhimu wa kuweka bima mali za Serikali sambamba na hilo Serikali ianzishe mfumo wa ufuatiliaji wa malipo ya bima ili kuhakikisha taasisi zote zinaziwekea mali za Serikali zinazostahiki kuwekewa bima na kuhakikisha taasisi hizo zinalipa kwa wakati. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ianzishe utaratibu wa kupitia upya miongozo yake kwa mashirika yake ya kibiashara hususani yale ambayo yanafanya kazi nje ya Zanzibar. Hatua hii itasaidia mashirika kujiendesha kibiashara na kuweza kushindana na kampuni nyengine za bima.

## Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umekusanya TZS 113.9 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 99.7 ya makadirio ya kukusanya TZS 114.2 bilioni. Kwa upande wa matumizi, ZSSF imetumia jumla ya TZS 127 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya kutumia TZS 179.2 bilioni.

**Mheshimiwa Spika;** Kiujumla ZSSF imekuwa ikifanya vizuri katika utekelezaji wake lakini Kamati inaishauri mambo mbali mbali ili izidi kufanya vizuri zaidi. Kamati inaishauri ZSSF kuimarisha mifumo ya teknolojia ya mfuko ili kuongeza ufanisi na huduma kwa wanachama.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ya Bajeti ilifanya ziara katika baadhi ya Taasisi na Mashirika kwa lengo la kujua utekelezaji wa bajeti zilizoidhinishiwa. Kamati imebaini yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC), Kamati imebaini kuwa Shirika linakabiliwa na changamoto kubwa na za muda mrefu ambazo zinaathiri utekelezaji wa Shirika. Baadhi ya changamoto ambazo Kamati imezibaini ni kiasi kidogo cha kodi kinacholipwa na wapangaji wa nyumba za Shirika hali inayolipelekea Shirika kukosa mapato na kushindwa kufanya matengenezo katika nyumba hizo. Vile vile, Shirika linakabiliwa na changamoto ya kuwepo wadaiwa sugu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Shirika la Nyumba kuchukua hatua za haraka za kukabiliana na wadaiwa sugu kwa mujibu wa Sheria iliyoanzishwa ili kuliwezesha Shirika kupata mapato yake na kuweza kujiendesha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuiliruhusu Shirika kuongeza kiwango cha kodi kwa nyumba zake kwa lengo la kuliwezesha Shirika kuongeza mapato ambayo yataweza kutumika kufanya matengenezo ya nyumba za Shirika. Kiwango cha kodi kinachotozwa sasa hakiendani na hali halisi.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika jengine ambalo Kamati ya Bajeti imeona itoe msisitizo kutokana na mchango wake katika kukuza uchumi wa nchi yetu ni Shirika la ZSTC ambapo Kamati imebaini kuwa linakabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa uwelewa mdogo wa madaraja kwa wakulima wa karafuu kwa kuhisi wanadhulumiwa kwa kupewa madaraja ambayo hawastahiki kupata kwa mujibu wa karafuu walizozipeleka.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri ZSTC kuanza kutumia teknolojia ya kisasa ili kuweza kutambua madaraja ya karafuu, hatua ambayo itaepusha malalamiko kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ni taasisi nyengine ambayo Kamati ya Bajeti ilitembelea. Kwa kuwa ZIPA inakabiliwa na changamoto ya Kuvamiwa kwa baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji kunarudisha nyuma jitihada za Mamlaka katika kuyaendeleza maeneo hayo. Kamati inaitaka Mamlaka kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa maeneo ya uwekezaji nchini na kujiepusha na vitendo vya uvamizi katika maeneo ya uwekezaji. Aidha, ZIPA waweke alama katika mipaka katika maeneo yote ya uwekezaji ili kudhibiti vitendo vya uvamizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokutana na Wakala wa Barabara ilibaini kuwepo kwa vitendo vya uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara kunakoathiri muonekano mzuri wa maeneo ya barabara hizo kwani wananchi huyatumia maeneo hayo kwa shughuli mbali mbali ikiwemo ujenzi holela. Aidha, suala la wizi na uharibifu wa alama za barabarani kunaathiri watumiaji na kukosekana kwa fursa kwa wananchi wanaotegemea alaama hizo kuwaongoza wanapokuwa barabarani. Katika kukabiliana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wakala kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuyahifadhi maeneo ya barabara pamoja na kutunza alama za barabarani ili barabara zetu ziwe katika muonekano mzuri pamoja na kuwaongoza watumiaji.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme (ZECO) lina majukumu ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa umeme Zanzibar. Kamati ilipotembelea Shirika la Umeme (ZECO) imebaini changamoto ya kuwepo baadhi ya taasisi za Serikali kutokulipa madeni yao ya umeme kwa muda mrefu. Kamati inaishauri Serikali kuja na mpango maalum wa kuitatua changamoto hii kwani ni ya muda mrefu, hivyo inahitaji ufumbuzi wa haraka.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Shirika la Bandari (ZPC), Kamati imebaini Shirika linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa magari ya ofisi kunalipelekea Shirika kupata hasara ya matengenezo ya kila siku na kunapelekea ugumu wa kazi za ufuatiliaji. Vile vile, bandari za Pemba kuna changamoto ya

kukosekana kwa mifumo ya kisasa ambayo inasaidia kufanya shughuli za bandari kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa suala la vitendea kazi ikiwemo vifaa vya kuendesha ofisi na usafiri vinahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kila siku za Shirika, Kamati inaishauri Shirika kuendelea kufuatilia upatikanaji wake kupitia bajeti zao ili kazi za Shirika ziweze kufanyika kwa ufanisi ikiwemo shughuli za ufuatiliaji. Aidha, Kamati inashauri Shirika la Bandari kuhakikisha mfumo wa e-Port unatekelezwa kwa ufanisi na uweledi mkubwa ili kuondokana na changamoto ya kutofikia malengo kwenye utekelezaji wa majukumu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Kamati imegundua changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yake kama vile kutokuwa na afisi zake za uhakika, uhaba wa wataalam, uhaba wa fedha za kuendesha ofisi pamoja na usafiri, aidha pia kuna changamoto ya Taasisi za Serikali kutokulipa gharama za kufanyiwa tathmini jambo ambalo linaikosesha mapato ofisi ya mthamini Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazisisitiza taasisi za serikali kulipa gharama za tathmini haraka mara baada ya kufanyiwa tathmini, vilevile Kamti inaiomba serikali kuipatia ofisi ya mthamini mkuu fedha za kuendesha ofisi kwa wakati, kuwapatia ofisi za uhakika, wataalam waliobobea, usafiri pamoja vifaa vya kutekeleza majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali inategemea ada ya uthamini kuwa ndio chanzo chake cha mapato, Kamati inaishauri Serikali kusimamia taasisi zake kulipia ada ya uthamini pindi wanapofanyiwa kazi zao ili kuifanya ofisi kukusanya mapato yake kutokana na kazi wanazozifanya. Vile vile, Kwa kuzingatia umuhimu wa mifumo ya kidigitali katika kuhifadhia taarifa, Kamati inaitaka Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali Zanzibar kujipanga kuwa na mifumo ya kidigitali ambayo itatumika katika kuhifadhia taarifa za tathmini.

**Mheshimiwa Spika;** Katika utekelezaji wa bajeti ZBC, Kamati imebaini ZBC imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha hususan fedha za miradi ya maendeleo. Mathalan, kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) 2021/2022, ZBC

ilijipangia kutumia jumla ya TZS 14.097 bilioni na ilifanikiwa kupata TZS 482.919 milioni tu kwa ajili ya kazi za kawaida na matumizi ya Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 3. Kwa upande wa miradi ya maendeleo kulipangwa kutumika TZS 12.127 bilioni kwa ajili mradi wa uimarishaji wa matangazo ZBC na hadi kumalizika kwa mwezi wa Machi 2022 hakukuwa na fedha zilizopatikana.

**Mheshimiwa Spika;** Ili kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali inapaswa kuja na mipango madhubuti ya kuhakikisha ZBC inajiendesha kibiashara. ZBC inapaswa kuwa na watendaji wa kutosha wenye kufanya kazi kwa weledi na ufanisi, kujikita katika matumizi ya teknolojia za kisasa pamoja na kuwezesha kupatikana kwa fedha na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya ZBC hususan uzalishaji wa vipindi, kurusha matangazo na kufuatilia matukio. Mipango hiyo iwezeshe ZBC kuweza kujitegemea na kujiendesha kibiashara na kufikia hatua ya kutoa gawio kwa Serikali badala ya kupokea ruzuku.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX), katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ilikadiria kutumia jumla ya TZS 1.921 bilioni lakini hadi kufikia Juni 30, 2023 matumizi halisi yalikuwa TZS 1.03 bilioni sawa na asilimia 54. Kati ya fedha hizo zilizotumika, TZS 167 milioni ni ruzuku kutoka Serikalini kwa matumizi ya kawaida (Subvention for other charges) ambayo ni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya TZS 421 milioni na TZS 1.525 bilioni ni makusanyo ya ZMUX ambayo ni sawa na asilimia 102 ya makadirio ya kukusanya TZS 1.5 bilioni.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kuiwezesha ZMUX kuimarika na hatimae kuweza kujitegemea na kujiendesha kibiashara, Serikali inapaswa iweke mikakati madhubuti ya kuimarisha ZMUX kwa kuingizia fedha kwa ajili ya kuimarisha ili ifikie uwezo wa kujitegemea. Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya ushindani wa kibiashara kutoka kwa watoa huduma wengine wa uunganishaji na usambazaji wa maudhui, Serikali inapaswa kuiwekea ZMUX kanuni na miongozo rafiki ya kibiashara ili iweze kujiendesha kibiashara na kumudu ushindani uliopo.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande mwengine Kamati ya Bajeti ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji katika baadhi ya Miradi ya Maendeleo pamoja na Programu mbali mbali iliyomo katika Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na kufanya ziara katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya Miradi na Programu hizo ni kama ifuatayo: Mradi wa Ujenzi wa Mundombinu ya Umwagiliaji maji, Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Usambazaji Maji Zanzibar, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa, Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa  Ofisi za Serikali, Mradi wa Mji Salama na Mradi a Ujenzi wa Ofisi za masheha, Mradi wa elimu ya juu kwa mabadiliko ya kiuchumi (HEET), Mradi wa ujenzi wa masoko ya mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini, Programu ya kuimarisha viwanja vya ndge na program ya ujenzi wa Ofisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kiujumla Programu na Miradi hiyo inakabiliwa na changamoto za kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi, kuchelewa kulipwa kwa fidia kwa wahanga wanaopisha miradi, kuchelewa kuingiziwa fedha za maendeleo. Hali hii inapelekea Miradi na Programu nyingi kutekelezwa kwa kasi ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kupanga miradi ambayo itawezekana kuanza kutekelezwa na kumalizika kwa wakati kwani kuchelewa kwa miradi hupelekea kuongezeka kwa gharama za miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**. Kwa kuwa Serikali ipo katika mpango wa kuleta maendeleo kwa kutatua changamoto za usafiri kwa haraka kupitia Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani pamoja na Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii sambamba na kuishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuongeza mashirikiano na Taasisi ama mamlaka zenye miundombinu yao katika maeneo ya utekelezaji wa miradi ya Barabara ili kuweza kufanya tathmini ya kina ili kuepusha wa miundombinu na hatiamae Serikali kupata hasara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Skuli wenye lengo la kuimarisha miundombinu na kuweka mazingira mazuri ya kufundishia, kujifunzia kwa ajili ya kutoa elimu bora na kuongeza ufaulu wa wanafunzi hasa wa masomo ya Sayansi. Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni kuwepo kwa bajeti ndogo katika Sekta ya Elimu ukilinganisha na mahitaji yaliyopo katika kuimarisha miundombinu ya elimu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti katika sekta ya elimu ili malengo ya kuimarisha miundombinu ya elimu nchini yaweze kufikiwa kwa kiwango kinachokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi mwengine ni Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Uhifadhi wa Chakula wenye lengo la kuhakikisha kunakuwepo kwa upatikanaji wa usalama wa uhifadhi na uhakika wa upatikanaji wa chakula kwa asilimia 65%.

**Mheshimiwa Spika,** Kuchukua muda mrefu kwa mchakato wa manunuzi hali inayopelekea kutokupatikana kwa fedha za mradi kwa wakati na uhaba wa vitendea kazi ikiwemo mafuta kunapelekea ucheleweshaji wa kazi hasa za ufuatiliaji wa nje ya ofisi ni miongoni mwa changamoto zinazoathiri utekelezaji wa mradi huo. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kukamilisha taratibu zinazohitajika ikiwemo za manunuzi ili waweze kupatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mradi wa Ujenzi wa Masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini, licha ya kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi huu kutokana na kutofautiana kwa makisio yaliyofanywa awali na kuongezeka kwa kazi katika masoko yote, Kamati ilipotembelea miradi yote ilishuhudia utekelezaji wake unaendelea vizuri. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuendeleza ujenzi wa masoko ambayo ni matumai ya Kamati kuwa, kukamilika kwake kutatoa fursa kwa wajasiriamali kuwa na maeneo maalum ya kufanya biashara zao na kujiingizia kipato.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Michezo Zanzibar, Kamati ilifuatilia utekelezaji wake na kubaini baadhi ya changamoto kama vile kuchelewa kwa fedha za kutekeleza miradi. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuipatia fedha Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo ili imalizie miradi hii na kufikia

malengo ya kuimarisha miundombinu ya michezo.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ambazo zimeshaanza kutekelezwa katika mradi huu. Aidha, Kamati inashauri Wizara na Taasisi nyengine inazoshirikiana nazo kufanya uchambuzi na kupitia mapendekezo ya wawekezaji na wajenzi kwa umakini ili kutatua changamoto zote zinazoibuka wakati wa kutekeleza mradi huu muhimu kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;** Katika Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB). Mradi wa HEET una thamani ya Dola za Marekani milioni 425 sawa na TZS 972 bilioni. Mradi huu una lengo la kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kujenga muunganiko imara kati ya elimu ya juu na soko la ajira. Hatua hii inaweza kufikiwa kwa kuwapatia wanafunzi ujuzi unaoendana na soko la ajira.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ndio kilichonufaika na mradi huu, kikiwa ni moja katika vyuo vikuu 14 vya Tanzania na ni taasisi pekee kwa Zanzibar iliyobahatika kunufaika na fedha za utekelezaji wa Mradi wa HEET, kimetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni 20 sawa na TZS 45.9 bilioni.

**Mheshimiwa Spika;** Mradi wa HEET ni muhimu sana katika kuimarisha sekta ya elimu, hivyo Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto ya kukosekana kwa malipo ya watendaji wa mradi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ishirikiane na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ili kupitia bajeti ya 2024/2025 kuwekwe kiasi maalum cha fedha kwa ajili ya malipo ya watendaji wanaotekeleza mradi huu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa uliotoa kwenye ripoti ya Kamati ya Febuari 2023 kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kiujumla Kamati imeridhika na utekelezaji wa maoni na ushauri wake uliyotoa kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri kwa upande wa Pemba. Aidha, Kamati inaisisitiza Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kusimamia utatuzi wa changamoto zote zilizobainika wakati Kamati ilipofanya ziara katika maeneo ya utekelezaji wa maoni na ushauri huo.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid kwa kutumia busara zako kuliendesha vyema Baraza hili la Wawakilishi kwa weledi mkubwa. Pia namshukuru Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika kwa kukusaidia vyema katika kutekeleza majukumu yako.


**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Maafisa Wadhamini, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizofanya kazi na Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yao mazuri na hatimae kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao muda wote wakati wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nachukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kumshukuru Mhe. Zawadi Amour Nassor ambae alikuwa mjumbe katika Kamati hii katika kipindi chote ambacho Kamati ilifanya kazi katika mwaka wa 2023/2024. Pia, nampongeza kwa uteuzi aliyoupata, namtakia mafanikio katika majukumu yake mapya ya Unaibu Waziri, Wizara wa Maji, Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishukuru kwa dhati kabisa Afisi ya Baraza la Wawakilishi na watendaji wake wote ambao waliweza kuisaidia Kamati katika kufanikisha kazi zake na kupatikana kwa ripoti yake kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa Wizara na Taasisi zote za Serikali kutekeleza maagizo na ushauri wa Kamati zote waliopatiwa ili kuimarisha utendaji wa Wizara na taasisi hizo na kupatikana kwa matokeo mazuri ya usimamizi wa Kamati kwa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa lipokee na kuijadili ripoti hii ili hatimae Serikali iende kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Baraza kwa ujumla. Naomba kutoa hoja.



……………………………….

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**